SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 34, Oktoba 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# PROF. MBARAWA AKAGUA MRADI WA SGR, AKUTANA NA WATUMISHI TRC



Na Mwandishi wetu.

Waziri wa Uchukuzi Mhe. Prof. Makame Mbarawa amefanya ziara ya kikazi katika Shirika la Reli Tanzania – TRC kuanzia Dodoma hadi Kigoma kuona maendeleo ya miradi, shughuli zinazofanywa na Shirika pamoja na kukutana na watumishi mkoani Tabora na Kigoma, Oktoba 2023.

Lengo la ziara lilikuwa ni kuona maendelea ya mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kuanzia Dar es Salam hadi Kigoma ambapo alipata pia fursa ya kuzungumza na wafanyakazi mkoani Tabora na Kigoma na kukagua

Inaendelea Uk. 2

## KICHWA KIPYA CHA TRENI YA SGR CHAWASILI NCHINI Uk. 3



# PROF. MBARAWA AKAGUA MRADI WA SGR, AKUTANA NA WATUMISHI TRC



Kaimu Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu Mhandisi Machibya Masanja akimuelezea Waziri wa Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa kuhusu mgodi wa kokoto kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora , eneo la Itigi mkoani Singida Oktoba 2023.

**Inatoka Uk. 01**

maendeleo ya maandalizi ya uwekaji wa jile la msingi la mradi wa SGR Tabora – Kigoma.

“Kazi ya ujenzi wa mradi wa SGR inaendelea vizuri japo kuna changamoto na ndio dhumuni hasa la kuja, changamoto kubwa kwenye mradi tuliyoiona ni kasi ya utekelezaji, tulitegemea tufike asilimia 22 kwa kipande cha Makutupora - Tabora lakini tumefika asilimia 12 kuna asilimia 10 zimepungua, naamini tukiweka mikakati mizuri tunaweza kukarudi kwenye mpango wetu kama kawaida” alisema Mbarawa

Prof. Mbarawa aliongeza kuwa kwenye miradi mikubwa popote Duniani changamoto zinakuwepo lakini cha msingi ni namna unavyoweza kusimamia changamoto na kuzimaliza ndio maana Serikali imetembelea mradi kuanzia Makutupora hadi Tabora ili iweze kuzungumza na mkandarasi kuhakikisha mradi unakamilika kwa wakati.

Mbarawa alisisitiza kuwa “Hakuna mpango wa kubadilisha mkandarasi kwakuwa mkandarasi yupo na anaendelea na kazi, Serikali inaendelea kutafuta fedha lengo ni kujenga reli hii ikamilike. Wale wanaopotosha naomba waache na niwatake TRC kumsimamia mkandarasi aweze kumaliza kazi kwa wakati” aliongeza Prof. Mbarawa

“Ni kweli kwamba kuna changamoto, cha kwanza kabisa tulichokifanya ni kumuelekeza mkandarasi aje na mpango mbadala wa kufidia muda uliopotea, pili tunaendelea na majadiliano kwa ajili ya kutatua changamoto” alisema Kaimu Mkurugenzi Mkuu Mhandisi Senzige Kisenge

Prof. Mbarawa akiwa katika ziara alipata fursa ya kuzungumza na wafanyakazi wa TRC Tabora na Kigoma, alieleza kuwa wafanyakazi ni sehemu muhimu sana ya Shirika kuhakikisha Shirika linatekeleza majukumu yake kikubwa ni kuwapa ari na morali wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa uadilifu na uaminifu kwa kufanya hivyo Shirika linaweza kufanya vizuri. Waziri Mbarawa alisisitiza juu ya umuhimu wa kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi utakaokidhi mahitaji ya uendeshaji wa treni za kisasa pindi mradi wa SGR utakapokamilika



Kichwa kipya cha treni kinachotumia nishati ya umeme kikishushwa kutoka kwenye meli kilipowasili bandari ya Dar es Salaam

# KICHWA KIPYA CHA TRENI YA SGR CHAWASILI NCHINI

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limepokea kichwa kipya cha treni ya umeme chenye namba ya usajili E6800-01 kilichoundwa na kampuni ya 'Hyundai Rotem Company' (HRC) kimewasili nchini Tanzania kutoka nchini Korea Kusini Oktoba 2023.

TRC iliagiza vichwa vipya 17 vya umeme kutoka 'Hyundai Rotem Company' (HRC) ya nchini Korea Kusini vyenye namba ya usajili E6800-01 hadi E6800-17 kwa ajili ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR. Mfumo wa uendeshaji unaotumika katika kichwa ni nishati ya umeme wenye msongo wa kilovoti 25 na kitakuwa na nguvu ya kilowati 5,000 sawa na nguvu ya 6,800 kwa kipimo cha 'Horse Power'. Kichwa kitakuwa na uwezo wa mwendokasi wa kilomita 160 kwa saa (160km/h), kuvuta na kulisha umeme kwenye mabehewa yasiyozidi 14 ya abiria kwa wakati mmoja.

TRC inatarajia kufanya majaribio ya kichwa cha treni kitakachotumika katika reli ya kiwango cha kimataifa kati ya Dar es Salaam na Morogoro  na baadaye Dar es Salaam hadi Dodoma, baada ya kukamilisha ukaguzi wa kichwa na mafunzo ya uendeshaji kwa madereva mapema mwezi Disemba 2023.

Mwezi Disemba 2023 TRC inatarajia kupokea vichwa vingine vitatu (3), mpango wa uletaji vitendea kazi utakuwa ukitekelezwa kwa awamu pindi uundwaji wa vitendea kazi unapokamilika. TRC imeshapokea mabehewa 35 kwa ajili ya uendeshaji wa huduma katika reli ya kiwango cha kimataifa.

Kufikia Septemba 2023 mradi wa SGR Dar es Salaam – Morogoro umefikia 98.6%, Morogoro – Makutupora umefikia 95.41%, Makutupora – Tabora umefikia 12.32%, Tabora – Isaka umefikia 5.02% na Mwanza – Isaka umefikia 41.95%, Mkandarasi kampuni ya CCECC yuko eneo la mradi kwa ajili ya maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi wa SGR awamu ya pili Tabora - Kigoma.

# WANANCHI MKOANI DODOMA WAPATA ELIMU KUHUSU KUANZA KWA MRADI WA DARAJA LA GODEGODE



Katibu Tawala mkoa wa Dodoma Bwana Ally Gugu (kulia) akizungumza na maafisa wa Shirika la Reli Tanzania alipokuwa akipokea taarifa ya kuanza kampeni ya uelewa kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode katika reli ya zamani (MGR) wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023

**Na Mwandishi wetu.**

Shirika la Reli Tanzania limefanya kampeni ya uelewa kwa wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode katika vijiji vya Godegode, Kimagai, Kisisi na Mgoma wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023.

Lengo la kampeni ni kuwapatia uelewa na utayari wananchi kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja na kuinua tuta la reli eneo la Godegode kutokana na changamoto ya uharibifu wa miundombinu unaosababishwa na mafuriko kipindi cha masika. Wananchi wameelezwa kuhusu fursa zitokanazo na mradi ikiwemo fursa za ajira, biashara pamoja na kupata uzoefu, pia wananchi wamefahamishwa masuala mbalimbali kuhusu usalama wa miundombinu ya reli na mambo ya kijamii yanayoambatana na mradi.

Meneja Mradi Msaidizi wa daraja la Godegode Mhandisi Enock Mayala ameeleza kuwa kupitia mradi wa daraja la Godegode “tunatarajia kuinua tuta na kujenga madaraja ili kupitisha maji na kuruhusu shughuli za uendeshaji wa huduma za treni kufanyika kwa kipindi chote cha mwaka, mradi unatarajiwa kufanyika kwa muda wa mwaka mmoja chini ya Mkandarasi kutoka China kampuni ya ‘China Civil Construction Corporation’ (CCECC)”.

Mhandisi Mayala ameongeza kuwa Mkandarasi yuko karibu kuanza mradi lakini kabla ya kuanza mradi upo utaratibu wa kuwashirikisha wadau na kuwapa elimu ya uelewa wa mradi na kuwafahamisha wadau kuhusu changamoto na fursa za mradi ikiwemo Shule ya Msingi Kimagai, Godegode, Shule ya Sekondari Godegode pamoja na wananchi wa vijiji vya Godegode, Kimagai, Kisisi na Mgoma kuwashirikisha

# WANANCHI MKOANI DODOMA WAPATA ELIMU KUHUSU KUANZA KWA MRADI WA DARAJA LA GODEGODE

Inatoka Uk. 4.

changamoto ya usafiri wakati wa masika na kuleta maendeleo katika vijiji vinavyozunguka mradi na nchi kwa ujumla.

“kwa kweli mradi huu tumeupokea vizuri kwasababu adha iliyokuwepo hapa ni kwamba kipindi cha masika hakupitiki na sisi tunategemea zaidi usafiri wa reli kwenda stesheni ya jirani Gulwe kwaajili ya kwenda wilayani Mpwapwa, kwahiyo kwa ujio wa mradi huu wa ujenzi wa njia na kujenga daraja tunaupokea vizuri sana” alisema Mwenyekiti wa kijiji cha Godegode Bwana Waziri Ramadhani

Bwana Waziri ameongeza kuwa elimu ya uelewa iliyotolewa kabla ya kuanza kwa mradi ni muhimu na itawasaidia wananchi kutambua mambo mbalimbali yanayoambatana na mradi na namna ya kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi

“kikubwa kilichozungumzwa ni ulinzi wa mali katika mradi pamoja na masuala ya ukatili wa kijinsia yanayoweza kujitokeza katika mradi, elimu hii imetufikia” aliongeza Bwana Waziri

Pamoja na mambo mengine mradi wa Godegode unatarajiwa kuleta fursa za ajira na biashara kwa wananchi wanaozunguka mradi ili kukuza uchumi wa nchi.

“Nitajitahidi kuhakikisha wananchi wanapata fursa za ajira na biashara kwa kuwapa elimu lakini pia itatusaidia kuwepo kwa usafiri wa uhakika kwaajili ya kusafirisha mazao yetu” alisema Mwenyekiti wa kijiji cha Mgoma Bwana Mengi Meshaki



Meneja Msaidizi wa mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode Mhandisi Enock Mayala akiwaelezea wananchi (hawapo pichani) wa kijiji cha Kimagai kuhusu kuanza kwa mrdi wa daraja la Godegode wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023.



Afisa Masuala ya Kijamii Bi. Mary Frank akiwaelezea wananchi wa kijiji cha Godegode kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii yanyopaswa kuzingatiwa wakati wa mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode, wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023.



Afisa Usalma wa Reli TRC Rajab Kisongo akiwaonesha wanafunzi wa Shule ya Msingi Godegode alama zitakazowekwa katika maeneo ya mradi kwa ajili ya usalama katika mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode katika reli ya zamani (MGR) wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023

# MATUKIO KATIKA PICHA



Wakili kutoka Shirika la Reli Tanzania Bwana Innocent Rweyemamu akiwapatia elimu ya masuala ya Sheria wanafunzi wa Shule ya Sekondari Godegode wakati wa kampeni ya uelewa kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode katika reli ya zamani (MGR) wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023



Mkuu wa kituo cha Polisi Reli Dodoma SP Anganile Msyani (kushoto) akiwaelezea wafanyakazi wa mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode kuhusu namna ya kujiepusha na ukatili wa kijinsia unaoweza kutokea katika mradi, wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi Dkt. Aly Possi (aliyeketi kati) katika picha ya pamoja na viongozi wa TRC, TARURA, TANROADS, NIT, na LATRA baada ya kufunga maadhimisho ya wiki ya usalama wa reli Oktoba 2023



Mkuu wa Wilaya ya Uyui Bwana Zacharia Mwansasu akimkabidhi cheti dereva wa bodaboda Bwana Ally Juma baada ya kuhitimu mafunzo ya usalama wa reli wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa reli yaliyofanyika mkoani Tabora, Oktoba 2023.



Katibu Tawala mkoa wa Dodoma Bwana Ally Gugu (kati) akiwa katika picha na maafisa wa Shirika la Reli Tanzania mara baada ya kupata taarifa ya kuanza kampeni ya uelewa kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja la Godegode katika reli ya zamani (MGR) wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Oktoba 2023



Afisa wa TRC Bwana Benson Mtui akiwapatia elimu wanakikundi cha Wayege kuhusu ulinzi na usalama wa reli mkoani Tabora, Oktoba 2023.

# TRC YAADHIMISHA WIKI YA USALAMA WA RELI

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeadhimisha wiki ya usalama wa reli iliyoambatana na kampeni ya uelewa kuhusu usalama wa reli katika uwanja wa Chuo cha Teknolojia ya Reli Tabora – TIRTEC mkoani Tabora kuanzia Oktoba 9 hadi 13, 2023.

Maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli yalifunguliwa na Mkuu wa Wilaya ya Uyui Bwana Zacharia Mwansansu Oktoba 09 na kufungwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi Dkt. Ally Possi Oktoba 13, 2023.

Maadhimisho yalibeba Kauli mbiu isemayo "Usalama Unaanza na Wewe, Chukua Tahadhari". Wadau walioshiriki maadhimisho ni Wizara ya Uchukuzi, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini - LATRA, Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia - TAZARA , Chuo cha Usafirishaji – NIT, Mamlaka ya Hali ya Hewa – TMA na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Katika ufunguzi wa Wiki ya Usalama Mgeni Rasmi alisema kuwa Serikali kupitia mashirika ya Reli Tanzania imekuwa ikitambua vyema umuhimu wa usalama na ulinzi wa miundombinu ya reli na wananchi kwa ujumla hivyo imeendelea kujenga miundombinu mipya na kuboresha iliyopo.

Mkurugenzi Mkuu LATRA Bwana Habibu Suluo alieleza kuwa wanachama wa Shirikisho la Mashirika ya Reli kwa nchi zilizomo kusini mwa Afrika (SARA) wamekuwa wakishirikiana katika kuunda kanuni na kutunga Sheria zinazodhibiti usalama.

"Wanachama wa moja kwa moja wa SARA yaanii LATRA, TRC na TAZARA tunashirikiana na wenzetu ambao wameanza mapema haswa kwenye kutunga Sheria za reli ili kuhakikisha Usalama unaheshimika" alisema Suluo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu kutoka Shirika la Reli Tanzania ambae ni Mkuu wa Chuo cha Teknolojia ya Reli Tabora Bwana Damas Mwajanga amesema kuwa TRC inaendelea kuimarisha usalama wa reli kwa kukarabati njia za reli, mabehewa, vichwa vya treni na kuongeza uelewa kwa wananchi.

"Shirika la Reli tumeendelea kuzingatia kanuni na miongozo ya kiusalama, kampeni za uelewa zimekuwa zikifanywa haswa katika miradi yetu ya SGR kuhusu usalama na ulinzi, ukarabati mkubwa wa mabehewa umefanywa na pia watumishi wa reli wanapelekwa kwenye mafunzo mbalimbali yanayo husu usalama" Amesema Bw. Mwajanga.

Akifunga maadhimisho Dkt. Possi alisema kuwa "Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kujenga mtandao wa reli nchi nzima na hivi punde tutaanza ujenzi wa kipande cha Tabora - Kigoma hizi zote ni kuwezesha nchi yetu kukua kiuchumi kwa kujenga miundombinu ya kisasa na yenye ulinzi na Usalama zaidi" alisema Dkt. Possi.

Mkuu wa Chuo cha Teknolojia ya Reli Tabora - TIRTEC Bwana Damas Mwajanga alieleza kuwa Shirika la Reli Tanzania limeendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza na kudhibiti ajali katika mtandao wa reli ambapo kupitia TIRTEC kimeandaa mtaala mahususi unaohusu usalama wa reli.

"Katika kuandaa wananchi kupokea mradi kampeni za usalama zimeendelea kufanyika, TRC kupitia Chuo cha Reli Tabora kimeandaa mtaala maalumu unaohusu Usalama wa Reli, mtaala utazalisha wataalamu watakaoongeza ufanisi na usalama wa shughuli za Reli" alisema Bwana Mwajanga.

Kampeni ya uelewa na uhamasishaji ilifanyika katika shule, masoko, vituo vya mabasi, vituo vya bodaboda, na maonesho kutoa elimu kuhusu masuala ya ulinzi na usalama wa reli ambapo wananchi walihamasishwa kuzingatia elimu waliyopewa ili kuepukana na ajali katika maeneo ya reli.

# WANANCHI WILAYANI MANYONI WAFAIDIKA NA FIDIA

**Na Mwandishi wetu.**

Zoezi la ulipaji fidia linalofanywa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) linaendelea kufanyika kwa wananchi na wengi waliopisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa wanajitokeza kupokea malipo katika kipande cha tatu kwenye mradi wa SGR Makutupora - Tabora, Shirika la Reli Tanzania linafanya malipo katika wilaya ya Manyoni mkoani Singida Octoba 2023.

Takribani Hundi 319 zimelipwa na zingine zinaendelea kulipwa, wananchi wanalipwa baada ya kupisha maeneo yao kwaajili ya ujenzi wa njia kuu ya reli SGR katika kipande cha tatu Makutupora - Tabora.

Afisa Miliki kutoka TRC Bw. Aristides Rwebangira amesema zoezi la ulipaji fidia linafanyika katika wilaya ya Manyoni katika vitongoji vinne mjini Manyoni, hadi sasa fidia imelipwa katika vitongoji vya Majengo, Tambukareli na Chang'ombe na zoezi linaendelea katika kitongoji cha Kipondoda pia litafanyika kata ya Muhalala katika kitongoji cha Gengeni na Kijiji cha Sukamahela katika kitongoji cha Chiwondo wilayani Manyoni mkoani Singida.

"Tunaomba wananchi waendelee kufika kwa wakati katika ofisi za serikali za Mitaa ambako timu ya TRC ipo kwaajili ya malipo ya fidia kwa wananchi, wafike na nyaraka zote muhimu zinazowezesha malipo kufanyika" ameongeza Rwebangira.

Mthamini kutoka Wizara ya Ardhi Bw. Iddi Muhibu amesema wananchi wanalipwa hundi za malipo kulingana na uthamini ulivyofanyika kwa kufuata taratibu na Sheria za uthamini wa Ardhi.

"Tunafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na timu kutoka TRC pamoja na viongozi wa serikali za mitaa kwahiyo zoezi hili linafanyika vizuri na Kila mwananchi anapata stahiki yake kwa malipo halali". amesisitiza Muhibu.

Mtendaji wa Kata ya Manyoni Mjini Bw. Ewani Watsoni Simkonda ameishukuru serikali na TRC kwa kuwezesha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa njia ya reli katika kipande cha tatu Makutupora - Tabora.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wote waliotwaliwa maeneo yao kupisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa katika sehemu zote ambako SGR imepita.



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania wakishirikiana na Mtendaji wa kata ya Manyoni kujaza fomu za wananchi kabla ya kuanza zoezi la malipo ya fidia ya ardhi na majengo kwa wananchi waliopisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa Makutupora - Tabora, mkoani Singida Oktoba 2023,



Mhasibu kutoka TRC Bi. Veneranda Mwita (kulia) akimsainisha kitabu cha malipo mkazi wa kitongojicha Chang'ombe Bwana Paschal John aliyepisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa Makutupora - Tabora katika ofisi ya kata ya Manyoni mkoani Singida, Oktoba 2023.

# WANANCHI TAKRIBANI 250 WALIPWA FIDIA KUPISHA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SGR KIPANDE CHA PILI MOROGORO - MAKUTOPORA



Maafisa wa Shirika la Reli Tanzania wakiandaa nyaraka za wananchi kabla ya kuanza zoezi la malipo ya fidia katika kijiji cha Mnase wilaya ya Chamwino mkoani Morogoro, Oktoba 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limelipa fidia kwa wakazi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha pili Morogoro - Makutopora Oktoba, 2023

Wananchi takribani 250 wamelipwa fidia katika wilaya ya Dodoma Mjini, Bahi, Mpwapwa na Chamwino jijini Dodoma, wananchi wengine waliolipwa fidia ni wa wilaya ya Kilosa na Mvomero mkoani Morogoro na bandaye walilipwa fidia wananchi wa wilaya ya Manyoni mkoani Singida.

Afisa ardhi kutoka TRC Benlulu Lyimo amesema maeneo yaliyolipwa fidia ni kwa ajili ya kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme na vivuko kwenye reli ya kiwango cha kimataifa.

"Fidia inayolipwa ni kwa mujibu wa Sheria, kanuni na Taratibu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzanian" alisisitiza Bi. Benlulu

Mtendaji wa Kata ya Mkonze wilaya ya Dodoma Mjini Bw.Matonya Kaondomo ameishukuru serikali na TRC kwa kulipa fidia kwa wakati ili wananchi wapishe ujenzi wa miundombinu ya reli ya SGR

"Wananchi wenzangu, fedha hizi mnazolipwa mkanunue maeneo mengine ili muone faida ya mradi" alisema Bw. Matonya

Bwana Richard Stephen mkazi wa mtaa wa Muungano B kata ya Mkonze wilaya ya Dodoma Mjini ameipongeza Serikali ya awamu ya sita kwa kuwalipa fidia kwa kiwango walichokuwa wakikitarajia.

"Eneo langu nilikuwa nalima mazao ya chakula, haya malipo niliyopokea nakwenda kununua eneo lingine" alisema Bw. Richard.

Zoezi la ulipaji fidia ni endelevu ili kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya SGR inakuwa ya kiwango cha kimataifa.




**BODI YA WAHARIRI**
**MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary**
**HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy**
**PICHA | Hassan Mbonde, Augustino Bulegea**